# TARGETER WINGS
## JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT
## GREDI YA NANE - 2024
## KISWAHILI

Wings 001

**Muda: Saa 1 dakika 20**

Jina ______________________________

Shule ______________________________

Nambari ya Usajili: __________________ Tarehe __________________

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.*

*(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.*

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| Swali | Upeo wa alama | Alama ya mwanafunzi | Kiwango cha utendaji |
| 1-30 | Alama 50 | | |
| Jumla | 50 | | |

**I. UFAHAMU WA KUSOMA**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 4:***

Fisi, sungura na ndovu walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Kutokana na uwezo wao kimapato, watoto wao walisomea katika shule ya Mabueni ya Mtepetevu. Wanafunzi wa shule hiyo walitembelewa na wazazi wao. Takribani kila mzazi alimbebea mwanawe chakula isipokuwa sungura. Walifanya hivyo licha ya kuwa watoto hao walikuwa wamerudi shuleni siku chache zilizopita.

Mkutanoni wazazi walizozana kuhusu maakuli shuleni, mavazi na hata mitindo ya nywele ya wana wao. Fisi na ndovu walikuwa mstari wa mbele kutaka wana wao wapewe mapochopocho. Wanyama wengi waliokuwa na wanao shule hiyo hawakuzingatia sana juhudi za wanao masomoni, kinyume na kawaida yao. Hata hivyo wengine waliona mbele wakapinga udekezaji huo.

Mzozano ulipokuwa ukipamba moto. Mwanawe sungura aliyekuwa akivaa kilalahoi aliingia mkutanoni. Baadhi ya wanyama walipomwona walishindwa kwani mkutano ulikuwa ni wa wazazi. Kijana aliketi na kuwasikiliza. Fisi alisimama na kusema, "Hatuelewi ni kwa nini watoto wetu hawali nyama choma, kima kwa chapati. Tunalipa! kwa nini wale bure na ugali tu?"

Kijana wa sungura alisimama na kusema, 'Hoja mnazotoa si..." Baadhi ya wazazi wakadakia na kusema "we! nyamaza u mtoto kazi yako ni kunyamaza na kuwapasha ujumbe wazazi wako baadaye." Kijana alikazana na hatimaye akapewa nafasi. "Kitanda msichokilalia, hamuwajui kunguni wake." Alipoulizwa walikokuwa wazazi wake alisema, "wazazi wangu waliliwa na simba sasa mimi ni mlezi wa wadogo wangu. Nimekuja kuwakilisha marehemu wazazi wangu." Wanyama wakashangaa.

"Ninapinga hoja ya mitindo ya nywele na mapochopocho kama chapati, watoto wafunzwe kutafuta elimu kwa bidii. Wakihimizwa watakuwa na adabu na hamu ya kusoma wakifanikiwa, baadaye watajitafutia raha maishani. Tuwafunze kujitegemea." Hatimaye wazazi waliomba msamaha na kumshukuru kwa mchango wake.

1. Watoto wa fisi, sungura na ndovu walikuwa wakisoma shule gani?



CamScanner

2. Hadithi hii imeonyesha kwamba baadhi ya wanyama hawajali juhudi za wanao masomoni. Andika mfano mmoja kutoka kwenye kifungu kuthibitisha kauli hii.

______________________________________________

3. Ikiwa kijana wa sungura hangefika mkutanoni unadhani kungetokea nini?

______________________________________________

4. Kwa nini kijana wa sungura alipuuzwa mkutanoni?

______________________________________________

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 5 hadi 8.***

Ingawa serikali ilipiga marufuku uchomaji makaa miaka mingi iliyopita, jambo la ajabu ni kuwa matumizi ya makaa yanazidi kuongezeka kila mwaka. Takribani asilimia sabini ya kawi inayotumiwa kila mwaka nchini, inatokana na miti.

Hata hivyo.kuna sababu nyinginezo zinazowafanya watu kukata miti na kuvuruga mazingira yetu. Matumizi ya mbao kuundia fanicha, ujenzi wa nyumba ni baadhi ya sababu zinazochangia ukataji miti. Sehemu ya ardhi yenye misitu aghalabu huwa na rutuba nyingi. Ongezeko la watu na mahitaji ya kiuchumi huwafanya wakulima kuziingilia sehemu hizi. Kukata miti na kujitengea nafasi ya kilimo.

Inakisiwa kuwa zaidi ya tani milioni moja za makaa zinatumiwa kila mwaka nchini. Ingawa wakenya pia hutumia gesi na mafuta taa kwa mahitaji yao ya kawi, asasi hizi mbili zimekuwa ghali mno kutokana na kupanda bei maradufu kwa bidhaa za petroli, kutokana na hali hii watu wengi mijini na mashambani wamelazimika kutumia kuni na makaa.

Serikali ilipopiga marufuku uchomaji wa makaa, maelfu ya watumiaji wa makaa hawakuelekezwa kwenye njia nyingine mbadala ya kujipatia kawi. Hivyo basi biashara ya makaa iliendelea kinyume cha sheria hadi leo. Hata hivyo, habari njema ni kuwa huenda misitu yetu ikapata nafuu kwani wakenya wengi wameanza kukumbatia kawi ya jua.

5. Kulingana na aya ya kwanza, jambo kubwa linalohatarisha misitu ni lipi?

______________________________________________

6. Ni sababu gani isiyochangia ukataji wa miti?
   A. Uhitaji wa shamba la kufanyia shughuli za kilimo. B. Uundaji wa fanicha.
   C. Matumizi ya miti katika ujenzi wa nyumba. D. Ujenzi wa barabara.

7. Kwa nini ni idadi ndogo tu ya watu inayotumia gesi na mafuta katika matumizi yao ya kawi?

______________________________________________

8. Kwa nini uchomaji makaa uliendelea hata baada ya kupigwa marufuku?
   A. Matumizi ya makaa yaliongezeka.
   B. Serikali haikuelekeza watu kwa sekta nyinginezo za kawi.
   C. Gharama ya maisha ilipanda kwa watu wa mijini.
   D. Matumizi ya kawi ya jua hayakuwa yamegunduliwa.

## II. UFUPISHO

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali 9 hadi 12.***

Baadhi ya vielelezo muhimu vya kulinda na kudumisha mila, utamaduni na desturi ya jamii yoyote ni nyimbo, ngoma, ngonjera, mashairi, muziki wa dansi, mavazi na mengineyo. ***Vielelezo hivyo sambamba na sanaa, lugha na michezo huwa kitambulisho cha taifa mbele ya macho ya ulimwengu***. Utambulisho huo hulifanya taifa husika kuwa linalojisimamia, lisilo na kasumba ya kigeni, lenye kujivunia hazina yake hiyo na uungwana wa raia wake.

Taifa lisilo na utamaduni ni taifa mfu. Katika miaka ya hivi karibuni, vielelezo hivyo vya utamaduni vimeanza kutoweka na hivyo kuathiri ustawi na malezi ya taifa letu hasa kwa vijana wetu. ***Moja kati ya sababu kubwa inayotajwa kusababisha hayo yote ni kuenea kwa matumizi ya teknolojia. Teknolojia imenasa kizazi cha vijana wa sasa ambao hujikita zaidi katika utamaduni wa kimagharibi***.

9. Andika habari kuu inayojitokeza katika aya ya kwanza kwa sentensi moja

______________________________________________

10. Kauli, "Vielelezo hivyo sambamba na sanaa, lugha na michezo huwa kitambulisho cha taifa mbele ya macho ya ulimwengu" imetumiwa katika kifungu. Fupisha kauli hii kwa maneno yasiyozidi 10.

______________________________________________

______________________________________________



CamScanner

11. Andika ujumbe wa kauli zilizokolezwa katika aya ya mwisho kwa sentensi moja

_______________________________________________

12. Andika kichwa kinachofaa kwa kifungu hiki

_______________________________________________

## III. SARUFI

***Soma kifungu kifuatacho ukijaza nafasi zilizoachwa wazi kutoka 13 hadi 17.***

Ni jambo linalovunja moyo kuona mitaa yetu imesheheni__13__ takataka za kila aina. Sharti tuelewe kuwa__14__ wa mazingira ni jambo__15__ lazima lishughulikiwe__16__kwa kuwa mazingira ni uhai, hatuwezi kamwe__17__ wito wa kuyatunza.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13. | A. mabiwi ya | B. mabunda ya | C. mabumba ya | D. makorija ya |
| 14. | A. kuhifadhi | B. malezi | C. uhifadhi | D. kutunza |
| 15. | A. ambao | B. ambalo | C. ambayo | D. ambacho |
| 16. | A. Zote | B. wote | C. yote | D. kote |
| 17. | A. kutathmini | B. kupuuza | C. kuchunguza | D. kuhimiza |

18. Chagua nomino dhahania kutoka kwenye kapu hili.




19. Sentensi: 'Mama anatukaribisha nyumbani kwao' ipo katika wakati na hali gani? ______________

20. Pigia mstari kitenzi kishirikishi kilichotumika katika sentensi ifuatayo:
Msitu huu u ni miongoni mwa rasilimali za nchi yetu.

21. Badilisha sentensi ifuatayo kutoka usemi wa taarifa hadi usemi halisi
Mwanafunzi alisema kuwa alishukuru mwalimu kwa mafunzo ya siku hiyo

_______________________________________________

22. Neno jito ni hali ya ukubwa ya neno mto.
Tunga sentensi ukitumia hali ya udogo wa neno: **Kitabu**

_______________________________________________

23. Maamkuzi, 'Alamsiki' hujibiwaje? ______________________

24. **Kanusha sentensi:**
Mbunge anawasilisha mswada bungeni:______________________

25. **Andika kinyume cha sentensi**
Mfalme huyu ni rafiki ______________________

26. **Andika wingi wa:** Umaarufu wa gavana wetu unatokana na uongozi wake mwema.

_______________________________________________

27. Kisawe cha heshima ni staha. Je, kisawe cha samaki ni ______________________

## IV. FASIHI

28. **Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali**

Lala mtoto lala x2
Mama anakuja lala.
Akupe maziwa lala.

Lala mtoto lala x2
Baba anakuja lala.
Akupenda toto lala.

Lala mtoto lala x2
Babu anakuja lala.
Akupe peremende lala.

a) Wimbo huu ni wa aina gani? ______________________



CamScanner

b) Eleza sifa tatu za wimbo wa aina hii.

______________________ ______________________

______________________

c) Andika wahusika wawili kwenye wimbo huu

______________________ ______________________

d) Eleza ahadi mbili ambazo zimeahidiwa katika wimbo huu

______________________________________________

______________________________________________

e) Unadhani wimbo huu unamlenga nani? ______________________

f) Tambua watu wawili ambao wanaweza kuimba wimbo huu

______________________ ______________________

## V. Tamthilia

**29.** ***Sehemu hii ina dondoo ambalo limetolewa kutoka kwenye tamthilia iliyoidhinishwa kwa wanafunzi wa gredi ya 8. Jibu swali la dondoo hili***

Mabula : Unapokula unabugia ukilacho chote mara moja? *(Mishi anamtazamo tu)* Utapaliwa! Unasikia? *(Mishi ananyamaza. Amebaki kumtazama tu. Mabula anainuka kutoka alipoketi. Anamwendea Mishi na kumshika sikio. Analisema kwa karibu lakini kwa sauti ile ile aliyokuwa akitumia)* unaelewa lakini?

Mishi : *(Anasonga nyuma hatua moja)* Mtu mzima! Huna haya kuniita na kuja kunisemea sikioni? Ungeyasemea huko ulikotoka.

Mabula: *(Anashangaa na kumtazama)* Aliyekuambia ninatoka kwenye masikio ya kusemewa ni nani?

Mishi: Kwani ni lazima kuambiwa kila jambo. Kwani mnakosa wa kuwasema huko kwenye hivyo vilabu vyenu? Mnadhani hatuyajui!

Mabula: Liseme basi unalolijua.

Mishi : *(Andika)* Ndiyo desturi yenu. Mnadhani sisi ni mabwege! Mabwege haswa *(kimya wanatazamana)*

Mabula: Yakiwepo hayo uombayo utayasema hivi usemavyo?

Mishi : *(Hataki kuyaendeleza mazungumzo haya)* Tafadhali niambie ulilonitia au kama halipo niache nizifuate shughuli zangu.

Mabula: *(Anamtazama kwa muda)* mimi nimerudi nyumbani kuja kujipumzisha lakini hakuna atakaye kujua kuwa ninahitaji walau tone la utulivu.

Mishi : *(Kwa kejeli)* Hatukulijua hilo bosi. Tungekuletea hata na usingizi wenyewe ukatwae mpaka utakapopenda kuamka.

a) Maudhui ni masuala yanazungumziwa katika kazi ya fasihi. Eleza masuala mawili yanayojitokeza katika dondoo hili.

______________________________________________

______________________________________________

b) Eleza sifa tatu za Mishi kulingana na dondoo hili

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**30.** a) Eleza mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

b) Tambua mandhari ya dondoo hili

______________________________________________

c) Andika mhusika mmoja katika dondoo hili

______________________________________________

# TARGETER WINGS

## JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT

# GREDI YA NANE - 2024

Wings 001

## SEHEMU B:

## KISWAHILI : INSHA

*MUDA: Dakika 40*

| | |
|---|---|
| **Jina** ______________________ | |
| **Shule** ______________________ | |
| **Nambari ya Usajili:** ____________ | **Tarehe** ____________ |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd. Email:info@targeterpublishers.co.ke*

**FUNGUA KURASA**

CamScanner

***Andika insha ya kusisimua itakayoanza kwa maneno yafuatayo:***

*Niliamka mapema tayari kuanza safari hiyo*..............................................................................